

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



TANGAZO LA MAENEO YA KUPANGA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kinapenda kutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na.	ENEO	MAELEZO/UKUBWA WA CHUNBA (m ²)	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Chumba Na. 02, Hosteli za Mabibo	58 m ²	Vinywaji Baridi na Vitafunwa
2.	Chumba Na. 03, Hosteli za Mabibo	47 m ²	Duka la Rejareja
3.	Chumba Na. 04, Hosteli za Mabibo	47 m ²	Kinyozi
4.	Chumba Na. 05, Hosteli za Mabibo	94 m ²	Mgahawa Mdogo wa Chakula
5.	Bweni Na. IV, Kampasi ya Mlimani	14 m ²	Kinyozi
6.	Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC), Mikocheni	Eneo linalohudumia takribani watu 200	Mgahawa Mdogo wa Chakula
7.	Kampasi ya Kunduchi	Eneo linalohudumia takribani watu 60	Mgahawa Mdogo wa Chakula
8.	Hosteli za Ubungo	Eneo linalohudumia takribani watu 100	Mgahawa Mdogo wa Chakula
9.	Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasaliano (CoICT), Kijitonyama	26.7 m ²	Duka la Rejareja

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 303 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi elfu kumi tu (10,000/=) kupitia 'Namba ya kumbukumbu' ambayo inapatikana Ofisi Namba 255 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua fomu na kurudisha ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika waombaji wote watataarifiwa juu ya matokeo hayo kwa njia ya barua.

Imetolewa na

NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO, UTAWALA

20.01.2020